


Muhtasari

- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia katika shughuli za uvunaji na ukaushaji wa mazao.
- Mvua za nje ya msimu zinazoendelea katika baadhi ya maeneo hazitoshelezi kwa kilimo cha mazao ya muda mrefu

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika hivyo kuimarisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. wakati ile migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika zaidi. Pia ukanda wa mvua uliendelea kuwa kaskazini mwa ziwa Victoria hali iliyopelekea upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani lilionekana katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Kwa wastani upepo ulivuma kutoka kusini hadi kusini mashariki, hali hiyo ilisababisha baridi katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilipelekea kupungua kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo ilipunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi ya Tanzania.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Julai 1- 10, 2019

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini magharibi hususan mkoa wa Mara ambapo yamepata mvua za nje ya msimu. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya 26 mm na 50 mm kama inavyojionesha kenye kielelezo.

Kwa kipindi hiki cha dikadi, hali ya ukavu iliyojitokeza katika maeneo mengi ya nchi imesaidia uvunaji, ukaushaji na utunzaji wa mazao kwa maeneo mengi ya nchi yanayopata msimu mmoja na misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Wakulima wamaejihusisha zaidi na shughuli za nje ya msimu ikiwa pamoja na uvunaji na ukaushaji wa mazao. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka zao la mahindi lilikua katika hatua ya kukomaa hususan mikoa ya Njombe, Mbeya na Iringa. Kwa upande mwingine mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Dodoma na Rukwa wakulima wanamalizia shughuli za uvunaji. Zao la ngano lilikua kati ya hatua ya kubeba na kukomaa kwa mikoa ya Njombe na Mbeya. Kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka zao la mahindi lilikua katika hatua ya kukomaa kwa upande wa mikoa ya Simiyu, Tanga, Moshi, Pwani na Mara shuguli za uvunaji zinaendelea. Shughuli za uvunaji wa mpunga zinaendelea katika Kwenye mikoa ya Mbeya (Usangu na Kyela), Ruvuma, Tabora, Kigoma, Morogoro Pwani, Simiyu na Shinyanga. Hali ya ukavu iliyojitokeza imepelekea kupungua kwa kiasi cha maji na malisho ya mifugo.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vimeendelea kupungua kutokana na kueundelea kwa kipindi cha ukavu na hali ya upepo hali hii imepelekea upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo .

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Katika siku kumi zijazo za mwezi Julai, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika zaidi hivyo kuimarisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa eneo la Afrika mashariki. Wakati migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika zaidi hivyo kuendelea kuruhusu ukanda wa mvua wa kuwa Kaskazini mwa ziwa Victoria. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi wakati upande wa kaskazini magharibi (karibu na pwani ya Somalia) joto litakuwa chini ya wastani, hivyo hali hii inatarajiwa kusababisha mkondo wa mgandamizo mdogo wa hewa kuwa katika maeneo ya ziwa Victoria. Aidha hali hiyo itasababisha upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Upande mwingine joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki linatarajiwa kuendelea. Hali hii inatarajiwa kuendelea kupunguza nguvu ya upepo wenye unyenyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi na ukanda wa ziwa Victoria katika nchi ya Tanzania. Kuendelea kuimarika kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia kunatarajiwa kusababisha kujitokeza vipindi vya upepo mkali na baridi katika maeneo mengi ya nchi.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na

Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja navisiwa vya Unguja na Pemba yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na hali ya mawingu kiasi.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi itasaidia kukomaa kwa mazao pamoja na shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao. Hata hivyo, hali ya ukavu itasababisha upungufu wa maji hususan kwa ajili ya malisho ya Wanyama. Wakulima wanashauriwa kutumia vipindi vya ukavu vinavyotarajiwa kwa shughuli za ukaushaji mazao mashambani pamoja na uvunaji. Vipindi vifupi vya mvua chache za nje msimu havitoshelezi kwa shughuli za upandaji wa mazao ya muda mrefu kama vile mahindi. Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maofisa ugani katika maeneo yao kwa ajili ya kupata ushauri zaidi.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana kuendelea kwa hali ya ukavu na upepo. Hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania